# OFISI YA RAISI
# TAWALA ZA MIKIO NA SERIKALI ZA MITAA
# MTIHANI WA KIDATO CHA SITA KABLA YA MTIHANI WA TAIFA
## 121/2 KISWAHILI 2

**MWONGOZO WA USAHIHISHAJI MTIHANI WA KABLA YA MTIHANI WA TAIFA**

1. Mwanafunzi aoneshe namna uhai wa fasihi unavyodhirika katika uwasilishaji
   a) Wakati wa uwasilishaji fanani na hadhira wanaonana ana kwa ana
   b) Wakati wa uwasilishaji huambatana na vitendo na ishara
   c) Wakati wa uwasilishaji hupokea mabadiliko ya papo kwa papo
   d) Wakati wa uwasilishaji huendana na wakati,mazingira na tukio lililopo
   e) Wakati wa uwasilishaji kunakuwa na ushirikishwa wa hadhira
   f) Fasihi simulizi huzaliwa, hukua na hufa.
2. Mwanafunzi katika swali hili aoneshe mawazo ya wataalamu kuhusu maana ya fasihi na atoe maana ya jumla katika kuhitimisha
   a) Mtaalamu Wellek na Warren wanadai kuwa fasihi ni jumla ya maandishi yote katika lugha fulani
   b) John Ramadhani,May Balisidya,Tigiti Sengo na Saifu Kiango wanadai kuwa fasihi ni hisi ambazo zinajifafanua kwa njia ya Lugha.Lazima pawe na mguso ndipo mwanafasihi aweze kuandika au kueleza jambo kifasihi.
   c) Wataalamu Peter Kirumbi,Aldin Mutembei na F.E.M.K Senkoro wao wanatazama kuwa fasihi ni kama sanaa ya lugha yenye ubunifu bila kujali kama imeandikwa au la.
   d) Mtaalamu Hills Summers anadai kuwa fasihi ni sanaa inayojumuisha zaidi maneno yaliyoandikwa,pia anadai kuwa fasihi ni maandiko bora ya kisanaa yenye manufaa ya kudumu
   e) Mtaalamu Mugyabuso Mulokozi anatazama fasihi kuwa ni tokeo la matumizi ya lugha kwa njia isiyoyakawaida ili kuleta athari maalumu.Fasihi hukiuka taratibu za kawaida za matumizi ya lugha katika sarufi maana na sauti ili kumvutia na kumuathiri msikilizaji au msomaji.
   f) Kwa ujumla,Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kiufundi kuwasilisha masuala mbalimbali yanayomhusu mwanadamu na maisha yake.
3. Mwanafunzi aoneshe athari chanya tano za udhamini wa Kazi za fasihi kwa msanii
   a) Udhamini huwasaidia baadhi ya wasanii kufanya tafiti za masuala mbalimbali yanayohusu jamii.
   b) Kuandaa Kazi mbalimbali kupitia msaada unaotolewa na wadhamini.
   c) Kuibua na kuendeleza vipaji vya wasanii.
   d) Kujipatia kipato kwa wasanii baada ya kuuza kazi zao.
   e) husaidia wasanii kuandika kazi zenye ubora na kiwango kutokana na kuwepo kwa ushindani katika Kuandaa kazi zao.
4. Mwanafunzi achambue vipengele vya fani kama vilivyotumika katika habari
   a) wahusika
   - wazazi
   - Nyangaswa
   - Vanesa
   - Mama Doto
   - Binti Cheupe
   - Ndugu
   - Walimu
   - Jamii
   - Rafiki
   - Masumbuko Sina

   b) Mtindo
   - Mtindo wa masimulizi

-mtindo wa nafsi (nafsi ya pili na tatu zimetumika)

c) Muundo

-muundo wa Moja Kwa Moja umetumika

d) Mandhari

-mandhari ya nyumbani(chumbani)

-mandhari ya mahakamani (ya kufikirika)

e) Matumizi ya lugha

- Tamathali za semi
  -tashibiha (wote walimuona kama kinyesi)
  -Sitiari(akawa piritoni)
  -Takriri(jamaa, jamaa)
  -Nidaa(loo!)
  -Mdokezo (hadi ukafikia kuhitimu kidato cha.......)
  -Mjalizo(kukuzaa,kukulea,kukusomesha)
- Methali
  -mchuma janga hula na wakwao
- Misemo na nahau
  -Alivuna alichopanda
  -walimtupa mkono
- Taswira
  -akawa piritoni(akawa mdogo)
  -kinyesi (kutokuwa na maana au thamani)

**FASIHI ANDISHI**

5. Utangulizi:Mtahiniwa aeleze maana ya maendeleo

Kiini

CHUNGU TAMU

(a) kupiga vita uongozi mbaya

Shairi la -Chungu Tamu

-Kwenye Mti Mkavu

b) Kutetea demokrasia ya kweli

Shairi -kademokrasia katoweka

c) Kuepuka vita

Shairi la-Daktari Askari

d) Kupiga vita dhuluma

Shairi la Chatu na Kuku

FUNGATE YA UHURU

a) Kupiga vita uongozi mbaya(Nataka Kusema,Fungate,Viongozi wa Afrika)
b) Kupiga vita matabaka(Maendeleo ya Imma,Wana wa Mungu)
c) Kupiga vita umaskini(Naona, Wengine)
d) Kupiga vita usaliti (Haki, Tumesalitiwa)
e) Kupiga vita dhuluma(Wizi, Joka la Mdimu)

KIMBUNGA

a) Vijana wawe na maadili mema katika jamii(Vijana wa Zanzibar, Wazazi)
b) Kupiga vita uongozi mbaya(Kibwangai,Kimbunga)
c) Kupiga vita rushwa(Rushwa)
d) Kufanya Kazi Kwa bidii(Kazi,Mkarafuu,Dumuzi)
e) Umuhimu wa elimu (Kisomo Cha Manufaa)

MAPENZI BORA

a) Kupiga vita chuki
b) Kupiga vita dhuluma
c) Kupiga vita ubaguzi wa rangi
d) Kuondoa mizozo katika jamii

*Utangulizi 02%*
*Kiini 16@02%*
*Hitimisho 02%*

6. Utangulizi

Mwanafunzi aeleze maana ya tamathali za semi za mlinganisho

KIMBUNGA

a) Tashibiha(tusiwe kama Mapunda,ulikuwa kama bubu,hukata kama mkasi,awe kama malaika)
b) Sitiari (bei imekuwa ndwele,beni kiti Cha ibilisi,usafi ni yake dawa, uvivuni angamizo,Amiga ni ngao Yako)
c) Tashihisi(Rushwa kajenga kambi na kuondoka hataki)

FUNGATE YA UHURU

a) Sitiari(Vijana nishati ya taifa,itikadi ya mapinduzi ni sukari,imma umekuwa bubu,waxed busara ya taifa,Sasa nani chano cha mji)
b) Tashibiha(ni kama jinga la moto,likatanda kama Moshi,niwachinje kamambuzi,watamba kama Chatu,nikawa kama wako baba na mama)
c) Tashihisi(Kiburi cha ukasuku tele kimejaa)

CHUNGU TAMU

a) Sitiari(ushairi ni sukari Tamu,utoto ni kito,dunia ni raha na tabu, wote weusi wa mkaa,mapenzi yakawa tiba vita ni Kazi,ndoa ni fumbo)
b) Tashihisi(kifo kimeniita,kicheche pia ameapa,huzuni imenisaliti,mapenzi hayana mpango,viganja vyake vilishirikiana na mashavu yetu)
c) Tashibiha(utaonekana kama kinyago cha kuchonga,nimekadibisha makofi mithili ya mvua,tukaswagwa kama mbuzi,mkali kama pilipili,mweusi kama kiatu cha jeshi,tuliyeyuka kama siagi juani)

MAPENZI BORA

a) Tashibiha(maana kifo daima hutokea kama mwizi,kama wiki kwa mchuzi,mfano kama mtoto,na tufue kama nguo,kama Mti Kwa mzizi,Kwa bidii Kama mchwa,mfano wa malaika,liwe kama yungiyungi)
b) Sitiari (Mapenzi kwangu uhai,dunia jagwa la kiu,maisha ni masihara,chuki uchafu wa moyo,mwenye chuki masikini,mapenzi ya la moyo,mapenzi ni miujiza)
c) Tashihisi(chuki imefua pingu,choyo kimetupa ganzi,roho zitie rutuba,mapenzi yana mwangaza,nyuso zimefanya njia,chuki ilie kwa aibu)

*Utangulizi 01%*
*Kiini 18@03%*
*Hitimisho 01%*

7. Mwanafunzi katika swali hili aoneshe mafunzo aliyoyapata kutoka katika riwaya alizosoma

USIKU UTAKAPOKWISHA

a) Tuwe na umoja katika jamii ili kuleta mabadiliko
b) Tuwe na subira katika maisha
c) Tuachane na mila potofu kwani ni kikwazo cha maendeleo
d) Mapenzi ya dhati ni liwazo na huleta furaha Kwa Kila mtu
e) Mvunja nchi ni mwananchi mwenyewe

VUTA N'KUVUTE

a) Tuache mila potofu Ili Kuepuka migongano katika jamii
b) Tuwe na umoja ili kufanikisha mapambano
c) Tuwe na mapenzi ya dhati Kwa wenzi wetu na nchi yetu
d) Tusiendekeze wivu uliopitiliza

MFADHILI

a) Tufanye kazi kwa bidi ili kuleta maendeleo
b) Tuonyeshe mapenzi ya dhati kwa wale wanaotupenda
c) Tukikosewa hatuna budi kutoa msamaha kwa wanaohitaji
d) Kunywa pombe si suluu ya matatizo
e) Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki

KUFIKIRIKA

a) Tusifanye mambo kwa dhanatu,tunatakiwa kufanya utafiti kwanza
b) Tujitume katika kazi ili kupata maendeleo
c) Katiba ya nchi lazima ifuatwe na watu wote
d) Tuwapeleke wagonjwa hospitali badala ya kutumia tiba za asili.

*Utangulizi 02%*
*Kiini 16@02%*
*Hitimisho 02%*

8. utangulizi

Mwanafunzi aeleze maana ya wahusika

Kiini

NGUZO MAMA

a) matendo ya uvivu ya wahusika
b) matendo ya umalaya
c) mafunzo ya ulevi
d) matendo ya usaliti
e) matendo ya dhuluma

MORANI

a)matendo ya usaliti na unafiki wa wahusika
b)matendo ya kishirikina
c)matendo ya umalaya
d) matendo uhujumu uchumi
e)matendo ya dhuluma

KIVULI KINAISHI

a)kitendo Cha BawabuII kupokea rushwa
b)vitendo vya dhuluma na uonevu
c)matendo ya usaliti na unafiki
d)matendo ya udikteta
e)matendo ya kishirikina ya kuwapumbaza Watu

KWENYE UKIGO WA THIM

a)matendo ya dhuluma
b)matendo ya usaliti na unafiki
c) kitendo Cha kuchaguliwa mchuma
d)Kitendo cha Viongozi kutokuwajibika.

utangulizi 02%
kiini 16 @ 02%
Hitimisho 02%